# ONGEZA KIPATO CHAKO NA KUKU WA KIENYEJI

*Mbinu Rahisi na Haraka za Kufuga Kisasa na kitaalamu kwa Mfugaji Anayeanza Biashara*

MUJAYA JONES MUJAYA

Toleo la kwanza, 2022
Hakimiliki @Mujaya Jones Mujaya, 2022

Mujaya Jones Mujaya
S. L. P 45019, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255715678122 au +255768678122
Baruapepe: ev.mujaya@gmail.com
Instagram: @mujayamj
Facebook: Mujaya MJ
Telegram: @mujaya
Twitter: @MujayaMJ

Uhariri, sanifu jalada na kurasa;
DL Bookstore
Simu: +255 786 163 013
Baruapepe: authors@dlbookstore.com
www.dlbookstore.com
Arusha, Tanzania

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA

Ni marufuku kuzalisha, kudurufu, kusambaza, kunakili au kutumia sehemu yoyote ya maudhui ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi na hatua kali za kisheria ikiwemo kifungo na faini zinaweza kuchukuliwa.

Maandishi, mpangilio na usanifu wa kitabu hiki ni mali ya mwandishi. Haki zote kuhusu kitabu hiki zipo chini ya Mujaya Jones Mujaya

# YALIYOMO

TABARUKU........................................................................................ v

DIBAJI.............................................................................................. vii

SHUKRANI........................................................................................ ix

UTANGULIZI..................................................................................... xi

SURA YA 1: FURSA ZILIZOPO KATIKA UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI.............................................................................................. 1

SURA YA 2: MAHITAJI MUHIMU YA MRADI.................................. 5

SURA YA 3: UPATE WAPI MTAJI?................................................. 11

SURA YA 4: BANDA BORA............................................................. 19

SURA YA 5: KUKU BORA............................................................... 31

SURA YA 6: UZALISHAJI................................................................ 43

SURA YA 7: UTOTOLESHAJI.......................................................... 47

SURA YA 8: JINSI YA KULEA VIFARANGA.................................... 53

SURA YA 9: MASOKO NA MAPATO YA MRADI WAKO................ 59

SURA YA 10: KWANINI WAFUGAJI WENGI WANASHINDWA?.... 67

SURA YA 11: HITIMISHO................................................................ 75

MAWASILIANO MUHIMU................................................................ 77

VITABU VINGINE VILIVYOANDIKWA NA MWANDISHI.................. 79

HUDUMA NYINGINE ZA MWANDISHI............................................ 81

WASIFU WA MWANDISHI............................................................. 83

# TABARUKU

Nimekiandika kitabu hiki kiwe mahsusi kwa watu wote ambao wanafuga au wanatazamia kuanza kufuga kuku wa kienyeji ili wajue mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wanaanza na kuendeleza mradi wao ili kupata faida.

Kitabu hiki kikawe hazina ya maarifa kichwani kwako na kikakupe pesa mfukoni mwako kupitia mradi wa ufugaji wa kuku wa kienyeji.

# DIBAJI

Ufugaji wa kuku wa kienyeji unapaswa kuchukua sura mpya kutoka ufugaji wa mazoea na kuwa ufugaji wa kibiashara. Fedha nyingi zitapatikana kwa wafugaji kama faida ikiwa mtindo na mtazamo wa kufuga kuku wa kienyeji utabadilika.

Kwa upande mwingine kuna haja kubwa ya kuendeleza mbegu za kuku wa kienyeji. Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, pamekuwa na tafiti za kisayansi zenye malengo ya kuboresha mbegu za kuku wa kienyeji ili kupata mazao mengi zaidi ndani ya muda mfupi.

Maendeleo haya yamepekelea mwingiliano mkubwa wa mbegu za kuku maeneo ya mijini na vijijini na kupelekea tishio la kupungua au kukosekana kwa kuku wa kienyeji kwenye masoko.

Kwa sasa karibu nusu ya kuku wanaouzwa kwenye masoko makubwa ni kuku wa kisasa au chotara tofauti na miaka michache iliyopita.

Kitabu hiki kinalenga kuleta ufumbuzi wa changamoto za wafugaji hasa wanaoanza, kuwapa njia ya kupata faida kubwa katika ufugaji wa kuku wa kienyeji, kuchochea ufugaji wa kuku wa kienyeji ili kutunza mbegu hii adhimu kwa vizazi vinavyokuja sambamba na kufungua masoko makubwa kwa bidhaa zitokanazo na ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Nimesukumwa na mwitikio pamoja na vilio vya watu wengi kupitia makala zangu kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji katika mitandao ya

kijamii kuweka kitabu hiki mikononi mwako ili kujibu sehemu kubwa ya maswali yako na kukuonesha njia unayopaswa kuipitia kuelekea mafanikio kwenye ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Nimewajibika kuacha urithi wa ujuzi, maarifa, na ufahamu wangu juu ya ufugaji wa kuku mahsusi kwa ajili ya kizazi hiki na kijacho. Nina imani maandishi ya kitabu hiki yatafika mbali kwa watu wengi kwa gharama nafuu.

Matarajio yangu utayasoma na kuyatekeleza mambo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Faraja na furaha yangu ni kuona umefanikiwa katika mambo yote mema unayofanya pamoja na ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Mujaya Jones Mujaya, Mwandishi.

# SHUKRANI

Namshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kuandika kitabu hiki. Hatua zote nilizopita nimeziona nyayo zake zimetangulia mbele yangu kunionesha njia na kuniwezesha.

Ninatoa shukrani za pekee kwa mke wangu na rafiki yangu wa siku nyingi Bi. Rafikiel Alfred Kimbwereza kwa kuniombea, kunitia moyo, kunisukuma na kunipatia huduma zote nilizohitaji hadi kukiweka kitabu hiki mbele yako.

Shukrani ziende pia kwa DL Bookstore waliofanya kazi kubwa ya uhariri, kusanifu mpangilio wa ndani ya kitabu, na jalada la kitabu hiki. Ninamshukuru Peter James Mkandi kwa usanifu wa nembo na machapisho ya Kuku Makini.

Bado ninadaiwa sana na familia yangu kwa kipindi kirefu nilipokuwa mbali nao na nilipolazimika kujitenga kwa ajili ya kazi hii. Najua mnanijali nami ninawapenda sana.

Ninatambua, ninathamini na kuheshimu pia mchango wa kila mtu aliyenisukuma, kunivumilia na kunielekeza hadi kitabu hiki kinakamilika.

Asante sana.

# UTANGULIZI

Umeamua kusoma kitabu hiki kwa imani au udadisi kwamba kuku wa kienyeji wanaweza kukuza kipato chako. Unatafuta njia ambayo itakuondoa kwa haraka katika changamoto za umaskini.

Katika jamii nyingi, kuku wa kienyeji na mazao yake yani nyama, mayai na vifaranga ni bidhaa zenye heshima ukilinganisha na aina nyingine za kuku.

Ni kweli taasisi za kisayansi na utafiti wa mifugo zimekuja na njia nyingi za kuboresha utagaji na uzalishaji wa nyama nyingi zaidi ya kuku kwa kubuni aina mpya za kisasa au chotara za kuku lakini bado kuku wa kienyeji wamekosa mshindani thabiti.

Kutokana na hitaji la kupata pesa za haraka bila kuangalia kwa umakini gharama na usumbufu uliotumika, wengi huona ni afadhali zaidi kufuga kuku wa kisasa au chotara kuliko kuku wa kienyeji. Lakini ukizishindanisha jamii hizi za kuku kwa kuzingatia faida na hasara za kila aina, utagundua kuku wa kienyeji wapo juu zaidi.

Sababu kubwa inayofanya kuku wa kienyeji wasionekane wana faida kubwa ni kutokana na ufugaji wa mazoea pamoja na kukosa mbinu sahihi za ufugaji wao ili kupata faida kubwa ambayo itaongeza pato lako kwa haraka.

Wafugaji hawafaidiki na kuku wa kienyeji kwa kuwafuga kiholela, kwa kuwafungulia nje waende wakajitafutie chakula wenyewe, watage wanapojua wenyewe, waatamie mayai popote pale, vifaranga vijipiganie maisha peke yao na wakae popote watakapopata.

Pia wafugaji wengine wameingia katika ufugaji wa kuku wa kienyeji kama vile wanavyofugwa kuku wa kisasa au chotara na wanatumia gharama kubwa za matunzo. Wanaingia gharama kubwa za ujenzi wa banda la kisasa, ununuzi wa vyombo na vifaa, uwekaji wa miundombinu ya banda, tiba ya magonjwa, gharama za chakula na uleaji wa vifaranga zimewaacha watu bila kupata faida kubwa mifukoni.

Hii ni fursa yako ya kujua mbinu rahisi za kufuga kuku wa kienyeji na mtindo wa matunzo utakaokupatia faida. Utamiliki biashara na mradi wa kuku wa kienyeji ambao utakuwezesha kuanza mavuno ndani ya muda mfupi.

Utapata njia za kupunguza gharama za ufugaji ili ukiuza kuku, mayai au vifaranga kwa bei ya juu upate faida kubwa sana. Utapata mbinu za kufuga kuku wa kienyeji wakati unaendelea na shughuli zako nyingine za uzalishaji mali.

# SURA YA 1

## FURSA ZILIZOPO KATIKA UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI

Ufugaji wa kuku wa asili haujapewa uzito unaostahili. Familia nyingi mijini na vijijini zinajihusisha na ufugaji wa kuku hawa kwa ajili ya kujipatia kitoweo au fedha wanapopata dharura au matukio maalumu.

Pamoja na faida hizo, ufugaji wa kuku wa asili unaweza kuwa ajira rasmi na chanzo kikubwa cha kipato. Kuna kanuni chache za msingi zinazohitaji kuboreshwa ili mfugaji apate manufaa.

Kabla hatujaenda mbali kuangalia kanuni hizo kwa undani, lazima tujue fursa za kifedha zilizopo katika ufugaji wa kuku wa kienyeji.

### FURSA ZA KUCHANGAMKIA

Ufugaji wa kuku wa asili una fursa nyingi sana ambazo unaweza kuzichangamkia haraka na ukatoka kimaisha. Kuna faida kubwa kutokana na mapato makubwa yanayopatikana kwa kutumia gharama ndogo zaidi.

Mazao ya nyama na mayai kutoka kwa kuku wa asili hupendwa zaidi na walaji ukilinganisha na aina nyingine za nyama au ndege. Nyama za kuku ni kitoweo adimu chenye heshima ndio maana huuzwa bei ya juu na hutumiwa sana kwenye matukio maalumu kama vile sherehe,

sikukuu na kukirimu wageni. Mayai na nyama za kuku wa kienyeji ni tamu na hufaa kwa aina nyingi za mapishi hasa ya kuchemsha. Pamoja na ladha yake pia mazao hayo huwa na harufu na rangi nzuri inayowavutia walaji.

Mazao ya kuku wa kienyeji yamepata umaarufu mkubwa kutokana na msukumo wa watu kuamua kuishi maisha ya kiafya ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Kuku wa asili wanaofugwa kwa njia rahisi za kienyeji bila vichocheo na madawa mengi ya viwandani hupelekea afya njema kwa mlaji.

Ni rahisi kuanza mradi wa kufuga kuku wa kienyeji sababu hawahitaji mfugaji awe na mtaji mkubwa. Mara nyingi mahitaji mengi ya kuku wa asili hupatikana kwa gharama nafuu. Kuku wa kienyeji wanaweza kutaga, kuatamia, kutotoa na kulea vifaranga vyao wenyewe hivyo wanaweza kuongezeka bila kuhitaji mfugaji aongeze fedha yake kwenye mradi.

Kuku wanatumia eneo dogo la ardhi na banda kutokana na udogo wa maumbile yao. Kwa upande mwingine, kuku wanazalisha kiasi kidogo cha takataka hivyo wanaweza kufugwa mahali popote.

Mtu yeyote bila kujali hali yake ya umri, maumbile au jinsia anaweza kufuga kuku kwa mafanikio. Kwa sehemu kubwa, elimu na ujuzi kidogo tu vinahitajika kuboresha ufugaji. Soko la kuku wa asili linakua kila siku na endelevu kutokana na ongezeko la idadi ya watu mijini na vijijini. Watu wanavyozaliana wanaongeza mahitaji ya chakula na kuku ni suluhisho la upatikanaji wa chakula.

## CHANGAMOTO UNAZOTAKIWA KUZIKABILI

Kuku wa asili wana ukuaji wa polepole ukilinganisha na aina nyingine za kuku. Kwa kawaida kuku wa kienyeji hutumia hadi miezi 6 au 7 ili aanze kutaga mayai au afikie uzito unaotosha kuuzwa sokoni.

Ukuaji wa polepole unasababisha mfugaji achelewe kupata pesa kutokana na kuuza mazao. Mfugaji analazimika kuwahudumia muda mrefu kabla hajaanza kurudisha pesa zake.

Ufugaji wa aina nyingine za kuku na ndege huwapa walaji mbadala wa mazao ya kuku. Kwa sehemu kubwa mayai ya kuku wa kisasa pamoja na nyama za kuku wa kisasa wa nyama zinauzwa bei ya chini.

Ushindani huu unaenda hadi kwenye urahisi wa ukuaji, wingi wa mayai, kuwahi kutaga au kuwa na uzito/maumbile makubwa. Kwa mfano: - kuku wa kienyeji mzuri anataga kwa wastani mayai 80 hadi 120 wakati kuku wa kisasa anataga mayai 250 hadi 300 kwa mwaka.

Kuna mchanganyiko wa mbegu au familia/koo za kuku wa asili katika jamii. Mchanganyiko huu unatokana na mwingiliano wa mbegu kwenye mfumo huria wa ufugaji. Kuku wa familia moja yani wenye undugu wa vinasaba wanaachwa kuzaliana bila kubadilisha jogoo.

Mchanganyiko huo unasababisha uwepo wa mbegu duni ya kuku. Kwa sehemu kubwa mbegu za kuku wa asili zina uwiano tofauti katika ukuaji, uzalishaji, ulaji wa chakula, uhimilivu wa magonjwa n.k ni vigumu sana kubainisha aina/familia ya kuku wa asili.

Changamoto kubwa inayosababishwa na mchanganyiko wa mbegu ni ukosefu wa taarifa sahihi wa jinsi ya kuwahudumia kibiashara. Ni vigumu kupata taarifa za kutosha kuhusu uzalishaji wa kuku wa asili ili mfugaji apange malengo ya kibiashara.

## JINSI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Changamoto za ufugaji wa kuku wa asili zinatakiwa kugeuzwa kuwa fursa. Mfugaji anatakiwa kutafuta mbinu na njia za kuzishinda changamoto zote katika mazingira yake na kubakia kwenye ufugaji kwa muda mrefu ili anufaike kibiashara.

Jinsi watu wanavyoacha kufuga kuku wa asili au wanavyoendelea na ufugaji wa mazoea ni fursa kwako kujijenga na kujiimarisha ili kuliteka soko kwa kuboresha na kukuza uzalishaji wako.

Ili upunguze changamoto za ufugaji wa kuku wa kienyeji, sharti uzingatie kanuni bora za ufugaji, usimamizi na utendaji wa kazi zako kila siku.

Miongoni mwa mambo ya msingi ya kuzingatia ni elimu sahihi itakayokupatia ujuzi stahiki. Wenye hekima walisema, *"mali bila daftari hupotea bila habari".* Taarifa ni nguvu, hivyo unatakiwa upate taarifa sahihi zikusaidie kufanya maamuzi ya ufugaji kibiashara.

**CHANGAMOTO**

*Ninapenda kusikia kutoka kwako, niambie ni changamoto gani kubwa zinakutisha usifuge kuku wa kienyeji? Sababu gani zinasababisha usianze kufuga?*

Unatakiwa ufuge idadi kubwa ya kuku. Jinsi idadi ya kuku inapokuwa ndogo ndipo changamoto za ufugaji na usimamizi zinapoongezeka. Udhibiti wa gharama za chanjo, madawa, chakula na mabanda n.k unategemea sana idadi ya kuku unaowafuga.